

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUMEYA USHINDANI

MUONGOZO KUHUSU UCHUNGUZI NA UTEKELEZAJI WA MAKOSA YANAYOKIUKA SHERIA YA USHINDANI (FAIR COMPETITION ACT, 2003) (SURA YA 285)

1.0 UTANGULIZI

- 1.1 Muongozo hii unalenga kutoa mwelekeo wa ujumla kwa umma na kwa wadau wa biashara, Idara za Serikali, taasisi za kisheria na zisizo za kisheria, walaji, taasisi za (au vyama vya) walaji Tanzania, na wadau wengine wote juu ya michakato ambayo TUMEya Ushindani (FCC) hufuata wakati wa kutekelezaji wa mamlaka yake chini ya Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003, (Cap.285), ambayo ni kuchunguza makosa na mienendo mbalimbali ya wafanyabiashara inayoyukiuka Sheria ya Ushindani. Hivyo basi, ni muhimu kuusoma kwa makini Muongozo huu pamoja na Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003 na Kanuni za Utaratibu wa Kushughulikia Makosa ya Kiushindani (FCC Procedure Rules, 2013).
- 1.2 Muongozo huu ni moja ya jitihada za TUMEya Ushindani katika kutoa ufafanuzi kwa Wadau kuhusu utaratibu wa kiuchunguzi unaofuatwa na TUMEpindi inapochunguza suala lolote linalohusu ukiukwaji wa Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003. Hivyo basi, Muongozo huu utakuwa unafanyiwa mapitio ya mara kwa mara na unaweza kubadilika wakati wowote kulingana na mabadiliko aidha yanayozingatia utendaji bora, (Best Practices, Sheria au Kanuni za Utaratibu wa Uendeshwaji wa Mashauri ya Tume. Kwa hali hiyo, Wadau wote wanashauriwa kuitembelea tovuti ya TUME(<http://www.competition.or.tz>) mara kwa mara ilikujua kama kuna mabadiliko yoyote.

- 1.3** Muongozo huu unaelekeza tu utaratibu wa kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko kuhusiana na ukiukwaji wa Sheria ya Ushindani kama yanavyoweza kuanzishwa chini ya kifungu cha 69 (1) na (2) ya Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003, kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 10 (1) na (2) cha Kanuni za Utaratibu wa Uendeshwaji wa Mashauri ya Tume, 2013.
- 1.4** Kwa kuzingatia umuhimu wa Mwongozo huu katika kutoa uwazi ni kwa jinsi na hatua gani TUMEya Ushindani (FCC) hutekeleza majukumu yake ya kufanya uchunguzi wake, ni muhimu kuisitiza kuwa Muongozo huu si mbadala wa Sheria yenyewe, na wala hauna hadhi ya kuwa Ushari wa Kisheria kuhusu masuala ya Ushindani. Vigezo vya kisheria ambayo TUMEya Ushindani hutumia wakati wa kutathmini ukiukaji wa sheria ya ushindani havijazingatiwa katika mwongozo huu. Hivyo basi, TUMEinawaasa Wadau na wale wote ambao wanadhani kwamba wao au biashara zao zinaweza kuchunguzwa na TUMEkwa sababu yoyote inayoambatana na uwezekano wa ukiukwaji wa Sheria ya Ushindani kutafuta ushauri huru wa kisheria.
- 1.5** Kwa ujumla, Muongozo huu unaweka bayana hatua mbalimbali za kiutaratibu ambazo TUMEhufuata pindi inapotaka kufanya uchunguzi wa ukiukwaji wa Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003. Muhtasari wa hatua husika ni kama unavyoonekana katika **Kielelezo 1.1** hapa chini:

Kielelezo 1.1 – Hatua za Kiuchunguzi FCC



2.0 MCHAKATO WA UCHUNGUZI WA SHAURI LINALOLETWA MBELE YA TUME

- 2.1** Mchakato wa uchunguzi wa matukio yanayoashiria ukiukwaji wa sheria ya ushindani ya 2003 ni jambo lenye msingi wake katika mfumo wa kisheria kama ulivyowekwa na Sheria ya Ushindani na Kanuni za TUME,2013.
- 2.2** Kama itakavyoelezwa zaidi katika Muongozo huu, mchakato wa uchunguzi huanzishwa na Tume, aidha kwasababu ya malalamiko yaliyowasilishwa rasmi mbele ya TUMEna mtu binafsi au kwa uamuzi wa TUMEyeneyewe chini ya kifungu 69 (1) au (2) ya FCA (kikisomwa pamoja na Kif. cha 10 (1) na (2) cha Kanuni za TUME, 2013.

3.0 Mamlaka ya TUME(FCC) KUFANYA UCHUNGUZI I

- 3.1** Katika jitihada za kuhimiza na kuhakikisha kuwa Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003, inafuatwa kikamilifu, kifungu cha 65 (2) (b) na (g) cha Sheria ya Ushindani kinaipa TUMEnguvu na mamlaka pana ya kuchunguza kero au mambo yanayozuia au kudhilisha ushindani, ikiwa ni pamoja na kuzuia urahisi wa makampuni kuingia na, au kutoka katika soko; kufanya uchunguzi wa kitafiti juu ya vizuizi katika soko au sekta ya uchumi vinavyo fifisha ushindani au vinavyo athiri uchumi kwa ujumla au katika sekta fulani na kutangaza matokeo ya uchunguzi huo.
- 3.2** Mazingira yanayoweza kuifanya TUMEkutumia mamlaka yake ya kuchunguza shauri ni kama ifuatavyo:
 - 3.2.1** FCC itatumia mamlaka yake, ama kutokana na malalamiko ya mlalamikaji huru (kwa mfano mshindani katika biashara, Mlaji au chama cha walaji, mtu mwingine yeyote, au kikundi cha watu, kuhusu madai ya ukiukwaji wa Sheria ya Ushindani, au kutokana na matakwa binafsi ya TUME(suo moto) mara inapobaini uwepo wa tatizo la kiushindani katika soko au uvunjifu wa dhahiri wa sheria ya ushindani.

- 3.2.2** Kwa mujibu wa kifungu cha 10 (1) (a), (b) na (2) cha Kanuni za TUME2013, malalamiko TUMEitashughulikia

malalamiko yote yanayowasilishwa mbele yake na watu huru kana kwamba yamewasilishwa na TUMEyeneyewe.

3.2.3 TUMEinazingatia matakwa ya utunzaji wa taarifa zote za siri kama inavyotakiwa na Kanuni za TUMEna, kwa hivyo, taarifa zote zinazopokelewa na TUMEkutoka kwa walalamikaji, hasa wasiopenda majina yao yawekwe hadharani, hubakia kuwa siri. Hili ni jambo muhimu kwa TUMEili kuleta ufanisi wa TUMEkatika kuchunguza malalamiko kwani kinyume na hapo Uchunguzi wowote unaweza kuhatarishwa endapo taarifa za siri zitawekwa hadharani kabla TUMEhaijachukua hatua stahiki za awali za kukushughulikia malalamiko husika. Hivyo basi, ili kusaidia TUMEkufanya uchunguzi wenye ufanisi, TUMEhuwataka walalamikaji kuwasilisha malalamiko yao na kuyachunguza kwa kuzingatia umuhimu wa usiri wa kila lalamiko hadi hapo TUMEinapoonavyema kuwasilisha hai ya kufunguliwa shauri (*statement of the Case*) kwa mtuhumiwa husika.

3.2.4 TUMEhaitatoa maelezo yoyote juu ya suala ambalo inalichunguza hadi inapokuwa imejiridhisha kuwa kuna suala la msingi la awali la uvunjifu wa sheria na, katika hatua hiyo, TUMEhuwasilisha hati ya kufunguliwa shauri la ushindani kwa Yule anayetuhumiwa kuihujumu sheria.

4.0 Nguvu na Mamlaka Mahususi ya TUME Wakati Kufanya Uchunguzi

Mbali na uwezo wa ujumla ambao TUMEimekabidhiwa kisheria kuchunguza masuala ya ushindani katika uchumi wa Tanzania, kwa mujibu wa kifungu cha 65 (2) ya Sheria ya Ushindani, FCC ina mamlaka maalum ya:

- (a)** Kuitisha nyaraka au taarifa mahususi zinazohusu kampuni inayotuhumiwa kukiuka sheria ya ushindani;
- (b)** kuingia katika majengo kwa kibali maalum (warrant) kwa lengo la kutekeleza sheria ya ushindani,

- (c) kuingia na kupekua kwa kibali maalum, nyumba, majengo au maeneo mengineyo, na
- (d) kumwita mtu yeyote kwa minajili ya kutoa ushahidi kwa mbele ya Tume.

4.1 Mamlaka ya Kuitisha Nyaraka au Taarifa

Mamlaka haya hutumiwa pale ambapo zipo sababu za msingi zinazoashiria kuwa mhusika amevunja sheria, hasa vifungu vifuatavyo: kifungu cha 8, 9, 10, au 11 (2) cha Sheria ya Ushindani. Kwa mujibu wa kifungu cha 71 (1) (a) na (b) cha sheria hii, FCC inayo mamlaka yakuitisha taarifa zitakazoonekana kusaidia katika uchunguzi wa suala lililo mbele ya Tume. Mamlaka hii hutumika kwa kuwasilisha mwito rasmi wa kuwasilisha taarifa (summons) kwa watuhumiwa au mtu mwingine yeyote; au kumtaka awasilishe taarifa ya maandishi au afike kwa ajili ya mahojiano rasmi na Tume.

4.1.1 Mamlaka FCC chini ya kifungu 71 (1) cha Sheria ya Ushindani inaweza kutumika kabla ya FCC kuwasilisha Hati ya Shauri la uchunguzi kwa Mhusika au baada ya kuwasilisha Hati hiyo. FCC inaweza pia kutumia mamlaka yake hata baada ya kuwasilisha au kutoa maamuzi ya awali ya Taarifa ya Uchunguzi (Provisional Findings) pale inapoonekana kuwepo haja ya kuendelea kutafuta au kufafanua ukweli juu ya jambo fulani litokanalo na maelezo au majibu kutoka kwa wahusika katika shauri linalochunguzwa na Tume.

4.1.2 Upana wa Matuzi ya Mamlaka ya TUMEchini ya Kifungu cha 71 cha Sheria ya Ushindani

- (a) TUMEitatumia mamlaka yake iliyopewa kwa mujibu wa kifungu cha 71 (1) na (2) ya FCA kama TUMEinaamini kwamba mtu anao (au Kampuni inao) uwezo wa kuipatia TUMEtaarifa, au kuwasilisha hati, nyaraka wa Tume, au kutoa ushahidi unaoweza kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Tume.
- (b) Katika suala hili, TUME inaweza, kwa njia ya wito (summons) na au bila wito, kumtaka mtu yeyote wa

kuwasilisha nyaraka au taarifa ikiwa taarifa au nyaraka husika inahusiana na jambo lolote muhimu linalochunguzwa na TUME. Kwa hiyo basi, TUME haiwezi kuwekewa vikwazo inapotaka kuchunguza taasisi, kampuni au watuhumiwa wa ukiukwaji wa sheria ya ushindani. Ilani ya kutaka taarifa za uchunguzi inaweza kuwasilishwa kwa watu wote wenye maslahi na shauri chunguzwa, kama vile washindani wenza, walalamikaji, wauzaji, na hata wateja; taasisi za Serikali , n.k.

(c) TUME inapotoa mwito wa kuwasilisha taarifa, inaweza pia :

(i) kuchukua nakala ya au sehemu ya taarifa ya nyaraka husika (Extracts) zitakazo wasilishwa mbele ya TUMEna mtu yeyote;

(ii) kumtaka mtu yeyote aliyewahi kutakiwa kuwasilisha nyaraka au taarifa mbele ya TUME (au afisa wake aliye kazini au aliyewahi kufanya kazi kwake)kuwasilisha maelezo ya ziada juu ya nyaraka husika au taarifa husika iliyokwishawasilishwa mbele ya TUME.

(iii)kama nyaraka husika hazikuwasilishwa, TUME inaweza kumtaka mtu aliyewahi kutakiwa na TUME kuwasilisha nyaraka mbele yake, kueleza, kwa kadiri ya imani na ufahamu wake, ni wapi, ambapo nyaraka husika yaweza kupatikana.

(d) Neno “nyaraka” ni pamoja na “taarifa iliyoandikwa katika mfumo wa aina yoyote”. Ufafanuzi huu ni pamoja na kumbukumbu zozote, kama vile ankara au takwimu za mauzo, ambazo zaweza kuwa zimehifadhiwa katika aina yoyote ya mfumo wa uhufadhi, ki-elektroniki au vinginevyo, kwa mfano, kwenye kompyuta. Nyaraka “maalum” ina maana ya nyaraka au taarifa zilizotajwa au ilivyoelezwa katika hati ya maandishi (wito). Mfano wa nyaraka kama hizo ni pamoja na, ankara, mikataba na taarifa za mikutano.

- (e)** Mtu aliyetakiwa kutoa ushahidi mbele ya TUME au kutoa taarifa kwa TUME kwa mujibu wa kifungu 71 (1) (a) na (c) ya Sheria ya Ushindani anaweza kufanya hivyo kwa njia ya hati ya kiapo.
- (f)** Kwa kuzingatia uwepo wa mamlaka ya kumtaka mtu yeyote kuwasilisha taarifa maalum mbele ya TUME, inaweza kuhitaji taarifa husika ziandaliwe na kuwasilishwa kama taarifa husika hazijaandaliwa na wahusika. Kwa mfano, mtu anaweza kutakiwa kuwasilisha mbele ya TUME taarifa zinazohusu maelezo ya soko analomiliki na kiwango cha umiki wake; au kutoa maelezo kuhusu soko husika kutokana na ufahamu wake na au, kwa kutumia maarifa yake, ujuzi na uzoefu wa wafanyakazi wake.

4.1.3 Utaratibu wa Uwasilishwaji wa Nyaraka na Taarifa mbele ya Tume:

- (a)** Iwapo TUME itatoa mwito kwa mtu au kampuni kufika mbele ya TUME kwa mujibu wa kifungu cha 71 (1) na (2), wito husika lazima uwe katika fomu inayotakiwa, yaani fomu FCC.7 na lazima kuonyesha:
 - (i)** majina la wahusika katika shauri;
 - (ii)** asili au undani wa habari wanayotakiwa kutoa;
 - (iii)** Mwito uwe umetolewa na kutiwa saini na Mwenyekiti wa TUME ya au Mkurugenzi Mkuu.
 - (iv)** Itolewe kwa mpokeaji anayehusika, au mtu aliyeidhinishwa kupokea, pia atatakiwa aandike jina lake / sahihi yake na nakala ya wito na uthibitisho wa kuwasilishwa utolewe na mhudumu karani / afisa kushuhudia kuwa mpokeaji au mtu mwenye mamlaka ya kupokea alipokea hati au Wito husika.

(b) Ikiwa mamlaka ya TUME chini ya kifungu cha 71 (1) cha Sheria ya Ushundani ina tekelezwa kwa kuwasilisha taarifa ya maandishi mengineyo isiyo na had ya Wito (Summons), taarifa ya maandishi lazima:

(i) Ieleze kwa muhtasari suala husika linalochunguzwa na madhumuni ya uchunguzi,

(ii) Itaje au kuelezea nyaraka au taarifa, au aina ya nyaraka au taarifa, zinazohitajiwa ;

(iii) Ibainishe makosa ambayo yanaweza kutendeka ikiwa mtu atashindwa kuzingatia au kutotekeleza anayotakiwa kutekeleza kwa mujibu wa matakwa na mamlaka ya uchunguzi ya TUME (kama ilivyoielezwa katika Sehemu ya 4.4 ya Muongozo huu);

(iv) Ibainishe muda na mahali ambapo nyaraka au taarifa husika itawasilishwa na namna ambayo itawasilishwa. Kwa mfano, ikiwa mtu atatakiwa kutoa taarifa au kuwasilisha nyaraka katika eneo maalum, kwa tarehe na kwa wakati fulani, taarifa zinazohitajiwa zinaweza kutolewa, kwa maandishi na au kwa maelezo yatakayo andikwa na afisa uchunguzi anaye husika. Mtu anayetoa taarifa atapata fursa ya marekebisho, kuongeza au kufuta maelezo yaliyoandikwa na atatakiwa kusaini yale yatakayokuwa yameandikwa kama maelezo yake. Kama mtu atawasilisha nyaraka, basi, TUME inaweza kumtaka aitolee maelezo ya ufafanuzi kimaandishi. Mtoa maelezo yeyote atakuwa na uhuru wa kuambatana na Wakili au mshauri wake wa masuala ya kisheria.

(c) Upelekaji na usambazaji wa nyaraka na miito kutoka TUME kwa walengwa unaweza kufanyika kwa njia zifuatazo:

- (i)** Kwa njia ya uwasilishwaji wa kawaida (yaani kwa mkono hadi ofisini kwa mhusika),
- (ii)** Kwa nia ya barua iliyosajiliwa posta na inayotaka mpokeaji kukiri kuwa ame- kupokea,
- (iii)** Kwa njia ya nukushi (fax) ikiambatana na ombi kuwa mpokeaji nakiri kupokea, au
- (iv)** Kwa njia ya ki-elektroniki (mf. e-mail) na ombi la kuambatanisha risiti ya upokeaji.

Hata hivyo, ikiwa nyaraka yoyote itawasilishwa nje ya muda wa masaa ya kazi ofisi ya TUME (yaani, Jumatatu- Ijumaa, 8:00-10:00) nyaraka husika itachukuliwa kuwa imepokelewa siku ya kazi inayofuata.

4.1.4 ANGALIZO:

Mtu yeyote (au kampuni) hatakuwa na kisingizio kuwa ameshindwa kutekeleza wito uliotolewa na TUME, chini ya kifungu 71 cha Sheria ya Ushindani, kwa misingi ya kwamba kutekeleza wito huo kungeweza kumfanya aonekane mkosaji au kumfanya mtu huyo awajibike kwa adhabu, isipokuwa taarifa, nyaraka au ushahidi utakaotolewa na mhusika hautaweza kutumiwa katika shauri jingile lolote dhidi ya mtu mwingine nje na shauri linaloendesha na TUME chini ya Sheria ya Ushindani.

4.2 Mamlaka ya TUMEya Kuingia na Kufanya Upekuzi

4.2.1 TUME ya Uchundania inayo mamlaka kisheria, kufanya upekuzi (search or inspection) wakati wowote inapokuwa ikifanya uchunguzi wa madai ya ukiukwaji wa sheria, kanuni, taratbu, na misingi ya ushindani.

4.2.2 Mamlaka ya TUME katika kufanya upekuzi huwezesha maafisa wake kuingia katika majengo (nyumba; ofisi, nk) na kuchukua (kukamata) nyaraka zozote zinazoonekana kuwa muhimu kwa ajilya ya kukamilisha uchunguzi wowote unaofanywa na Tume.

4.2.3 "Jengo au Majengo" kwa ujumla ni dhana inajumuisha "majengo yote yote yanayotumiwa kwa shughuli mbalimbali yakiwemo majengo ya biashara, ofisi, maghala au stoo zinazotumiwa kuhifadhi nyaraka, bidhaa, nk, au jingo lolote linalohusiana na mambo ya kampuni au ambamo nyaraka zinazohusiana na mambo ya kampuni inayochunguzwa zinaweza kuwa zimehifadhiwa. Hii inamaanisha kuwa katika suala la upekuzi, hata nyumba binafsi zinaweza kufanyiwa upekuzi. Neno "Majengo" linajumuisha pia magari yoyote au vyombo vya moto (vessels).

4.2.4 Upana wa Matumizi ya Mamlaka ya Kufanya Upekuzi

(a) Mamlaka ya TUME ya kuingia ndani, na kufanya upekuzi katika majengo yoyote hutekelezwa kwa kuzingatia misingi ya haki hasa pale inapoonekana kuwa ziko sababu za msingi za kuamini kwamba mhusika amekiuka vifungu vya Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003, (hasa kifungu cha 8, 9 au 10 cha sheria husika, na mhusika huyo anazo katika milki au udhibiti wake, nyaraka yoyote ambayo inaweza kusaidia TUME katika utekelezaji wa majukumu yake.

(b) Afisa uchunguzi anapoingia katika jengo lolote kwa ajilya upekuzi anaweza kumtaka:

(i) Yeyote katika jengo husika kumpatia nyaraka, hati au taarifa yoyote ambayo afisa uchunguzi huyo anaona inahusiana na jambo lolote muhimu kwa uchunguzi anaoufanya. Kwa mfano, mfanyakazi katika jengo husika anaweza kutakiwa kumpatia afisa uchunguzi husika miniti

za mikutano yoyote iliyowahi kufanywa na kampuni husika na washindani wake, shajara (diaries) za wakurugenzi WA Kampuni, taarifa (data) ya mauzo, au Ankara za mauzo. Nakala za hati au nyaraka yoyote kama zinaweza kuchukuliwa na afisa uchunguzi,

- (ii)** Yeyote katika majengo kutoa maelezo ya hati au nyaraka zilizopatikana au anazowasilisha kwa Afisa upekuzi anayehusika. Kwa mfano, mfanyakazi aweza kutakiwa kutoa maelezo ya maingizo (entries) katika Ankara au kutoa nywila (passwords) za kompyuta.
- (iii)** Yeyote katika jengo husika, kutoa maelezo, kwa kadri ya ufahamu wake binafsi na anavyoamini, ni wapi ambapo hati au nyaraka yoyote muhimu kufanikisha uchunguzi husika, au inayohusiana na jambo lolote muhimu kwa uchunguzi huo, yanaweza kupatikana.
- (iv)** Yeyote katika jengo husika, kutoa taarifa yoyote, ambayo imehifadhiwa katika mfumo wa aina yoyote ya ki-elektroniki na jinsi ya kuipata taarifa hiyo katika namna inayosomeka, ikiwa Afisa uchunguzi husika anaona kuwa taarifa hiyo inahusiana na jambo lolote muhimu kwa uchunguzi, na kwamba inapasa kuwasilishwa katika namna ambayo inaweza kusomwa na kuweza kuwa kuchukuliwa.
- (v)** Afisa upekuzi ataweza kuchukua hatua nyingine yoyote ambayo yanaonekana muhimu na inayofaa ili kuhifadhi nyaraka au kuzuia uwezekano wa vifaa, au ofisi kuingiliwa na mtu yeyote kipindi chote cha upekuzi. Hii ni pamoja na kuhitaji kwamba majengo ya (au sehemu yoyote ya majengo, ikiwa ni pamoja na ofisi, majalada, na kabati za ofinisi) kufungwa kwa muda kama hatua muhimu ili kuwawezesha wapekuzi

kukamilisha zoezi husika bila kuingiliwa. Muda wa kipindi chote cha kupekua na, hata muda wa kufunga sehemu za ofisi au jengo husika zisiingiliwe na mtu yeyote, hakipaswi kuzidi masaa sabini na wawili (72), isipokuwa pale ambapo Kampuni au mtu husika ataridhia upekuzi uendelee zaidi ya masaa 72 au ikiwa upatikanaji wa taarifa na nyaraka unacheleweshwa kwa sababu yoyote, kama vile kutopatikana kwa mtu ambaye anaweza kufungua ofisi husika.

- (vi)** Afisa uchunguzi (upekuzi) anaweza kuzuia, kukamata, na kuchukua pamoja naye vifaa vyovyote ambavyo anaona ni muhimu, pale anapoingia na kupekua jengo lolote kulingana na mamlaka aliyonayo kisheria. Kwa mfano, anaweza kuchukua vifaa vinavyobebeka, kama vile kompyuta, nk.
- (vii)** Afisa upekuzi atalazimika kuandikisha orodha ya vitu vyote vilivyochukuliwa naye na kuikabidhi nakala moja kwa mmiliki au mwakilishi wa mmiliki wa jingo au ofisi husika, mwishoni mwa ukaguzi, au kama iwezekanavyo na kwa vyovyote vile, katika muda wa siku tatu (3) siku za kazi kutoka mwisho wa siku ya kufanya upekuzi. Nyaraka zote zilizochukuliwa zutapaswa kurejeshwa ndani ya muda muafaka.
- (viii)** Afisa uchunguzi atatakiwa kutunza kwa ukamilifu kila nyaraka ya ushahidi iliyopatikana kutoka katika kompyuta na nyaraka nyinginezo zote zilizopatikana kutoka katika jengo lililopekuliwa katika namna ambayo itakidhi matakwa ya uadilifu wa kutunza nyaraka au taarifa.

4.2.5 Utaratibu wa Kuingia Katika Jengo au Ofisi Yoyote kwa Ajili ya Upekuzi

- (a)** Pale ambapo TUME itafikia uamuzi wa kufanya upekuzi katika jengo au ofisi yoyote ili kupata taarifa au kukamata nyaraka, TUME haitawajibika kwa namna yoyote ile kutoa taarifa ya awali kwa mhusika au mmiliki wa jengo au ofisi husika.
- (b)** Mwenyekiti wa TUME, au Mkurugenzi Mkuu wa Tume, atawasilisha maombi ya upande mmoja (*ex-parte application*) mbele ya Baraza la Ushindani kuomba Baraza litoe hati au kibali kitakacho ruhusu Afisa Uchunguzi wa TUME, akiambatana na afisa wa jeshi la polisi, cha kuingia na kufanya upekuzi katika majengo na kuchukua nakala au kuchukua nyaraka humo. Vilevile, Afisa uchunguzi husika anaweza kuambatana na mfanyakazi wa TUME mwenye ujuzi wa fani ya ufundi wa kompyuta au wataalam wa sekta ambao wanaweza kutekeleza majukumu maalum chini ya usimamizi wa afisa husika wa polisi.
- (c)** Hati au Kibali cha Kupekua (*Search Warrant*) kitabainisha kwa ukamilifu majengo au ofisi husika itakayopekuliwa na kitabaki halali hadi moja kati ya mambo yafuatayo yawe yametimizwa:
 - (i)** Hati au kibali husika kimetumika na kufanikisha malengo yake;
 - (ii)** Hati au kibali husika kufutwa na mtu ambaye alikitoa au, na mtu mwenye mamlaka sawa naye aliyekitoa,
 - (iii)** Lengo au sababu za kutoa kibali au hati husika kupitwa na wakati.
 - (iv)** Muda wa uhai wa Hati au Kibali husika kumalizika.

- (d)** Wakati kuingia katika majengo yoyote kwa ajili ya ukaguzi, afisa utekelezaji na watu wote wenye mamlaka ya kuandamana naye, atatakiwa kuwasilisha ushahidi wa utambulisho wake pamoja na ushahidi wa mamlaka ya Hati au Kibali cha upekuzi mara tu anapowasili kwenye maingilio ya jengo au ofisi husika.
- (e)** Afisa wa polisi, na maafisa wengine wowote walioandamana na Afisa wa Upekuzi watakao kuingia ndani ya jengo wataruhusiwa kuingia na vifaa vyote wanavyodhani kuwa muhimu na, katika hali yoyote ya upinzani dhidi ya upekuzi halali, Polisi husika na maafisa wa upekuzi wataruhusiwa kutumia nguvu isiyopitiliza (yenye busara ndani yake) ili kufanikisha lengo lao la kuingia na kufanya upekuzi uliokusudiwa. Vifaa husika ni kama vile vifaa ambayo yanaweza kutumika kwa kuvunja kufuli) kama vile vifaa vinavyoweza kutumika ili kuwezesha upekuzi wa kompyuta, nk).
- (f)** Mwenendo mzima wa kuingia na kupekua ofisi au jengo lolote utazingatia matumizi ya njia bora ambazo ni pamoja na:

 - (i)** Kuzingatia haki za msingi za binadamu za watu binafsi;
 - (ii)** Haja ya kuwa na mashuhuda wa kujitegemea, hasa walinzi wa amani, au uwepo wa watu wawili watu wazima ambao ni mashuhuda wa kujitegemea (binafsi), ila tu pale ambapo kupata watu kama hao itakuwa vigumu.

4.3 Mipaka Juu ya Matumizi ya Mamlaka ya Upelelezi

- 4.3.1** Mamlaka ya kutaka taarifa au nyaraka ziwasilishwe mbele ya Tume, kama ilivyobainishwa katika Sehemu ya

XII ya Sheria ya Ushindani, haihusiani na utoaji wa taarifa zenye kinga ya kisheria (privileged information), yaani:

(a) Mawasiliana kati ya mshauri wa kitaalamu wa kisheria na mteja wake, au

(b) Taarifa au mawasiliana yaliyofanyika kuhusiana na, au katika kutafakari uwezekano wakufungua, kesi za kisheria na kwa ajili ya kesi hizo. Hii ina maana kwamba mawasiliano na mawakili wa ndani (in-house lawyers) au wa nje, ikiwa ni pamoja na wanasheria wa kigeni, yanaweza kunufaika na kinga kama hii,

(c) Mawasiliano yoyote ambayo kwa namna yoyote yasingeweza kutolewa mbele ya mahakama kwa misingi kuwa yana kinga ya kisheria

4.3.2 TUME haitatumia, kama ushahidi, nyaraka yoyote iliyopatikana wakati wa upekuzi ikiwa nyaraka hiyo ina taarifa zenye kinga kisheria.

4.4 Makosa Yanayohusiana na Mamlaka ya Upelelezi

4.4.1 Kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani, ni kosa la kisheria ikiwa Kampuni au mtu yeyote anayetakiwa na TUME kutoa ushirikiano wakati wa shughuli za uchunguzi wa shauri la kiushindani kukataa kutoa ushirikiano. Hii ni pamoja na mtu yeyote ambaye -:

(a) Hali aikijua atatoa taarifa za uongo au zakupotosha au ushahidi unaopotosha huku akijifanya kutekeleza wito wa TUME uliomtaka kutoa taarifa au nyaraka mbele ya TUME.

(b) bila ya udhuru halali anakataa au inashindwa kuzingatia wito, chini ya kifungu cha 71 cha Sheria ya Ushindani.

4.4.2 Kuzuia utekelezaji halali wa sheria ya ushindani pia kunaweza kumfanya mtu au Kampuni kushitakiwa chini ya sheria nyingine zinazohusika, kama vile Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16.

5.0 Upembuzi wa wa Malalamiko, Kufungwa kwa Jalada, na Kurudishwa au Kuahirishwa ya Upelelezi

5.1 Malalamiko yote yanayopokelewa na TUME kuwasilishwa kwanza kwa Kamati ya Upembuzi kwa ajili ya kuhakikiwa ilikubaini, miongoni mwa mambo mengine, kama yanayohusiana na ushindani; yanaendelea katika chombo kingine kama vile katika mahakama yoyote, chombo cha usuluhishi, au ni suala lililokwisha fanyiwa maamuzi (res-judicata), au ni suala ambalo kwa uhalisia wake, si busara kutumia rasilimali za TUME wakati husika kulishughulikia.

5.2 Kulingana na vipaumbele vya TUME na rasilimali zilizopo, na au sababu nyingine kama inaweza kuelezwa na TUME, Mkurugenzi Mkuu wa TUME anaweza kulifunga jalada la uchunguzi au kusimamamisha au kuahirisha uchunguzi unaoendelea.

5.2.1 Ikiwa Mkurugenzi Mkuu anaamua kuifunga, kuahirisha, au kukataa kuchunguza lalamiko au kusitisha uchunguzi kwa misingi ya kutokidhi haja ya vipaumbele vya TUME, au kama itakavyokuwa kwa vyovyote vile, basi, TUME itawajulisha walalamikaji rasmi kwa maandishi, ikiwa ni pamoja na kuweka bayana sababu kuu za kutoendelea na uchunguzi wa shauri hiska. Kiasi cha undani wa maelezo atakayotoa kitategemeana na mazingira ya kila shauri. Kama shauri lilikuwa limefika mbali kiuchunguzi vivyo hivyo na maelezo ya kina yatahitajika ikiwa TUME haitaendelea nalo.

5.2.2 Pale ambapo mlalamikaji rasmi haridhiki na uamuzi wa kusitishwa kwa uchunguzi au vinginevyo kama ilivyoielezwa katika aya ya **5.2.1** hapo juu, mlalamikaji atapata fursa ya kupeleka suala hilo kwa TUME kwa ajili ya uamuzi na TUME itatoa nafasi kwa mlalamikaji

kuwasilisha kwa maandisha maoni yake ndani ya kipindi kitakachoelekezwa na TUME.

5.2.3 Ikiwa shauri limeondolewa katika uchunguzi, au umekuwepo uamuzi wa kutolichunguza shauri lililowasilishwa kwenye TUME, au ikiwa mlalamikaji rasmi ameshindwa kuwasilisha maoni yaliyoandikwa ndani ya muda uliowekwa na TUME, malalamiko husika yatachukuliwa kuwa yameondolewa mbele ya TUME.

5.2.4 Iwapo itaonekana kwamba kitendo au mwenendo wa soko unaolalamikia hauna madhara au uwezekano wa kuleta madhara katika ushindani, pande zinazohusika zitapewa taarifa na sababu zitakazoelezea kwamba TUME haichukua hatua yoyote zaidi kuhusu malalamiko yaliyowasilishwa mbele ya TUME.

6.0 Utoaji wa Hati ya Kufunguliwa Shauri la Uchunguzi

6.1 Ikiwa upembizi wa malalamiko yaliyowasilishwa mbele ya Tume utaonyesha kuwa lipo shauri la msingi linalokidhi haja ya kupatiwa majibu, TUME, itawasilisha rasmi Hati ya Shauri la Ushindani, kwa watakaohusika na Hati hiyo itaweka bayana mambo yafuatayo:

6.1.1 Maelezo muhimu ya awali yanayoweza kubainisha ukweli wa shauri au malalamiko husikai, na

6.1.2 Vifungu muhimu ya sheria vinavyodaiwa kukiukwa na wahusika (walalamikiwa).

6.2 Baada ya kuwasilishwa kwa Hati ya Kufunguliwa Shauri la Ushindani kwa walalamikiwa, Shauri husika litaendelea kwa uchunguzi zaidi. Hatua hii inajulikana kama hatua ya kwanza ya uchunguzi ambapo TUME hukusanya taarifa muhimu ili kuiwezesha, miongoni mwa mambo mengine:

6.2.1 Kufanya tathmini ya awali ya masoko husika, na kupata uelewa wa jinsi ushindani ulivyo katika masoko hayo; na

6.2.2 Kupata uelewa wa nafasi ya, na tabia na, au mwenendo wa ki-tabia wa mtu au Kampuni ambayo ni mshukiwa wa uchunguzi, katika soko husika.

6.3 Maofisa wa Uchunguzi wanaweza kuitisha, kukusanya na kutathmini taarifa au takwimu muhimu za kiuchumi za kampuni, zitakazo baini ukweli wa jambo ambalo linachunguzwa, kwa mfano, sehemu ya asilimia ya soko inayomilikiwa na kampuni inayotuhumiwa kuhujumu ushindani; takwimu zinazohusiana na bei, sera ya Kampuni husika kuhusi jinsi ya upangaji bei za bidhaa au huduma zake; taarifa za ki-fedha n.k.

6.4 Maofisa wa Uchunguzi wanaweza kuitisha mikutano ya majadiliano na pande zinazohusika ili kupata ufafanuzi au maelezo kuhusu tabia inayolalamikiwa na madhara yake na ushindani.

7.0 Utunzaji wa Siri (Confidentiality)

Mtu yeyote ambaye atatoa taarifa, maoni, au maelezo ya awali au ziada kwa TUME wakati wowote shauri linalochunguzwa likiendelea, atatakiwa kubainisha waziwazi ni sehemu ipi ya maelezo au taarifa yake angelipenda isitolewe nje ya TUME na hivyo atajaza taarifa husika katika Fomu ya taarifa za siri , yaani FCC.2.

8.0 Uandaaji wa Taarifa (Ripoti) ya Ndani ya Upelelezi (Uchunguzi)

8.1 Mara tu baada ya kumalizika kwa uchunguzi wa awali, timu ya Maofisa wa Sheria wa Tume waliohusika na uchunguzi, itatakiwa kuandaa na kuwasilisha Ripoti ya Ndani (Internal Investigaton Report (IIR)) kuhusu uchunguzi wake.

8.2 Ripoti Ndani Uchunguzi (IIR) iliyoandaliwa na timu ya Maofisa wa Uchunguzi, itakuwa kinga ya kisheria ya upendeleo kwa watendaji wa ndani ya TUME tu na hivyo haiwezi kutolewa kwa mtu wa nje, wala haitawasilishwa kwa yeyote nje ya TUME.

8.3 Maofisa wa Timu ya Uchunguzi watatoa mapendekezo na maoni yao ya kisheria ambayo yanaweza kuwa msingi wa uamuzi wa TUME wa aidha kutekeleza matakwa ya kisheria ya Sheria ya Ushindani pale ambapo sheria imekiukwa au vinginevyo.

9.0 Uandaaji wa Ripoti ya Utekelezaji

9.1 Kwa kuzingatia maoni yaliyowasilishwa na Timu ya Maofisa wa Uchunguzi katika Ripoti ya Ndani ya Uchunguzi (IIR) Timu ya Wanasheria wa ndani wa Tume itaandaa Ripoti ya Ndani ya Utekelezaji wa Sheria (Internal Enforcement Report (IER)) ili kutoa ushauri wa kisheria kwa TUME.

9.2 Ripoti iliyoandaliwa na Timu ya Wanasheria wa TUME itakuwa kwa matumizi ya ndani tu na itakuwa na kinga ya kisheria (privileged Report) ikiwa na maoni ya kisheria na mapendekezo yatakayo wasilishwa kwa TUME kuhusu utekelezaji wa Sheria na hatua zinazopaswa kuchukuliwa kulingana na kiwango cha ukiukwaji wa Sheria ya Ushindani.

10.0 Uwasilishwaji wa Maamuzi ya Awali ya TUME

10.1 Maamuzi ya Awali ya TUME (Provisional Finding (PF)) ni maamuzi ambayo TUME (kupitia Makamishna wake) hutoa kama mtizamo wao wa awali na mapendekezo yao kuhusu hatua inazoelekea kuchukua mbeleni ikiwa TUME haitapata taarifa au ushahidi utakazokinzana na ushahidi uliokusanywa unaolithibitisha kosa au makosa yaliyobainika kutendwa na Mlalamikiwa. Maamuzi haya ya Awali humpatia mtuhumiwa au mlalamikiwa nafasi ya kulifahamu shauri liliochunguzwa na TUME kwa upana wake, ikiwa ni pamoja na ushahidi wote ambao TUME imezingatia katika kufikia maamuzi yake ya awali, na hivyo humwezesha aweze kujibu rasmi na kikamilifu tuhuma zote dhidi yake kimaandishi na au, kwa mdomo au kuomba nafasi ya majadiliano ya maridhiano (settlement discussions).

10.2 'Maamuzi ya Awali' yanayotolewa na Makamishna lazima yawe na vielelezo vyote vya ushahidi uliozingatiwa na sababu zilizopelekea TUME kuamua kwa jinsi itakavyokuwa imeamua.

10.3 'Maamuzi ya Awali' yanapaswa kubainisha kwa udhahiri ukweli wa mambo (facts) na tahmini ya kisheria na kiuchumi ya TUME ambayo itapelekea TUME kuona kuwa Mhusika alikiuka sheria. Pia, TUME itaweka bayana hatua yoyote inayopendekeza kuchukua, kama vile kuweka adhabu kifedha, na / au kutoa amri ya kuacha ukiukwaji wa sheria mara moja, ikiwa TUME inaamini kuwa ukiukwaji huo bado unaoendelea, na sababu za TUME kuchukua hatua kama hiyo.

10.4 Kadhalika, 'Maamuzi ya Awali' ya TUME yataweka muda muafaka ndani ambao Kampuni inayotuhumiwa itahitajika kuwasilisha kwa TUME. kwa maandishi majibu ya Maamuzi ya Awali ya TUME. Muda huo utapangwa na Makamishna waliolichunguza shauri husika.

10.5 Katika hatua hii, TUME pia itatoa mwito wa kufika mbele ya TUME kwa aliyetumiwa (yaani Mpokeaji wa 'Maamuzi ya Awali') kama angependa kusikilizwa au kuwasilisha maombi ya kufanya majadiliano ya maridhiano na TUME, hii ikiwa ni moja ya haki zake ambazo zitaelezwa ndani ya Maamuzi ya Awali ya TUME.

11.0 Uwezekano wa Kupatiwa Fursa ya Kulipitia Jalada la Uchunguzi na Jinsi ya Kulinda Taarifa za Siri

11.1 Baada ya kuwasilisha Maamuzi ya Awali ya TUME kwa Mlalamikiwa, TUME, kutokana na maombi yatakayokuwa yameletwa na kampuni inayotuhumiwa au wakili wake, na chini ya malipo ya ada yoyote ambayo inaweza kuhitajiwa, itatoa nafasi kwa Kampuni husika au mwakilishi wake kulipitia kwa kulisoma jalada lote lenye taarifa za uchunguzi wa shauri husika. Hii ni kuhakikisha kwamba Kampuni husika inapewa nafasi ya kuandaa vizuri utetezi wake dhidi ya madai kuwa imevunja Sheria ya Ushindani.

11.2 TUME itatoa muda na nafasi nzuri kwa Kampuni au mtu aliyepokea Maamuzi ya Awali ya TUME kukagua nakala za nyaraka zote zinazohusiana na jalada la uchunguzi ambazo kimsingi hazina kinga ya kisheria kama zitakavyokuwa zimehifadhiwa katika jalada la uchunguzi la TUME. Hizi ni nyaraka ambazo zinahusiana na mambo yaliyomo katika Maamuzi ya Awali ya TUME, ukiondoa taarifa zozote za siri na Nyaraka za Ndani za TUME.

12.0 Utoaji wa Tangazo kwa Umma na Mwito wa Kuwasilisha Maoni

12.1 Kwa mujibu wa Kanuni za Tume, 2013, mara tu baada ya kutolewa kwa Maamuzi ya Awali ya TUME, TUME itatakiwa kutoa tangazo kwa umma (Public Notice) kuhusina na uamuzi wa awali uliotolewa na TOME kuhusu shauri husika la ushindani lililombele yake. Taarifa hiyo itachapishwa katika tovuti ya TUME na kuchapishwa kwenye magazeti yanayosomwa kwa wingi, na;

- 12.2** TUME itaatoa mwito kwa mtu yeyote ambaye ana sababu za msingi kuwa aliathirika na kitendo kinacholalamikiwa, kuwasilisha maelezo ya kimaandishi ya jinsi alivyoathirika. Maelezo hayo yatatakiwa kuwasilishwa kwa TUME ndani ya kipindi maalum ya muda kitakachokuwa kimwekwa na kutangazwa na TUME.

13.0 Uwasilishwaji wa Maelezo/ Majibu Kuhusu Maamuzi ya Awali ya TUME

- 13.1** TUME inapotoa 'Maamuzi ya Awali' itachukua hatua ya kuwaalika Walalamikiwa (Respondents) ili kujibu hoja zilizopo katika Maamuzi hayo ya Awali 'kwa maandishi'. Hata hivyo, Mlalamikiwa halazimishwi kuwasilisha majibu kama mhusika anakubaliana na tuhuma husika.
- 13.2** Uwakilishi wa utetezi wa kimaandishi utakuwa ni moja ya fursa za kutolea maelezo au maoni kuhusu mambo yote yaliyoelezwa katika nyaraka ya 'Maamuzi ya AWali ya TUME'. Maoni au maelezo/mafafanuzi, yaweza kuwa juu ya maelezo au taarifa ambazo TUME ilizingatia au tathmini ya kisheria na kiuchumi iliyofanywa na TUME kama itakavyookuwa inaonekana katika maamuzi yake ya awali.
- 13.3** Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha tetezi wa kimaandisha itakuwa imebainishwa katika Maamuzi ya Awali ya TUME na muda huo utazingatia mazingira ya kesi husika.
- 13.4** TUME itampatia 'mlalamikaji wa awali' nakala ya Maamuzi ya Awali ya Tume (toleo lisilo la siri) kuhusiana na matokeo ya muda ya shauri husika.

14.0 Maombi ya Kusikilizwa na TUME (Oral Hearing)

- 14.1** TUME itatoa nafasi kwa wote waliopokea 'Maamuzi ya Awali ya TUME' ya kuhudhuria na kusikilizwa na TUME, ikiwa ni pamoja na kupata fursa ya kutoa maelezo ya mdomo juu ya ufafanizi wowote wa jambo au hoja yoyote iliowasilishwa kimaandishi mbele ya TUME.
- 14.2** TUME itawahimiza Wahusika wote kuchukua fursa hiyo ya kuhudhuria na kusikilizwa na hivyo watapaswa kuthibitisha kuwa wangependa kufanya hivyo.

- 14.3** Fura ya kusikilizwa na kutoa utetezi wa mdomo itakuwa nafasi ya kipekee kwa Mtuhumiwa au yeyote Yule, kuonyesha masuala yaliyo umuhimu kuhusiana na shauri husika ambayo ameyaaanisha katika utetezi wake wa maandishi.
- 14.4** Kama kanuni ya jumla, jambo lolote litakalokuwa limebainishwa wakati wa kutoa utetezi mbele ya TUME, litazingatia tu yale ambayo tayari yameainishwa katika utetezi wa maandishi uliokwisha wasilishwa mbele ya TUME.
- 14.5** Mlalamikiwa (Respondent) atakuwa na haki ya kuwakilishwa na Wakili au washauri wa kisheria au watu wengineo wenye nafasi ya kumsaidia katika kuwasilisha utetezi wake wakati wa kusikilizwa, lakini kwa kuzingatia kikomo au mipaka yoyote ya kiidadi ya wahudhuriaji inayoweza kuwekwa na TUME.
- 14.6** Mwishoni mwa wakati wa kuwasilisha hoja za mdomo, TUME, inaweza kuuliza maswali kwa ujumla au maswali mahusui kwa kutaka ufafanuzi na maswali hayo yatakuwa kwa njia ya maandishi.
- 14.7** TUME itatunza taarifa (rekodi) ya kimmandishi ya uwakilishi na utetezi wa mdomo itakayotolewa kwa wahusika kwa lengo la kuthibitisha usahihi wake na utambulisho wa taarifa yoyote ya siri ambayo wasingependa itolewe hadharani. Hata hivyo, TUME haitakubali madaai yoyote ya usiri yasuiyokuwa na maelezo makamilifu.
- 14.8** TUME itazingatia yote yaliyoandikwa katika mawasilisho ya utetezi wa kimaandishi pamoja na hoja zote zilizotolewa kwa mdomo mbele ya TUME na kufanya mapitio tena ya shauri zima pamoja na Maamuzi yake ya Awali ilikuona ikiwa Maamuzi hayo bado yanaungwa mkono na ushahidi uliopo, hata baada ya kuzingatia utetezi uliowasilishwa mbele ya TUME. Kama ushahidi uliopo bado unakidhi haja ya TUME kuendelea na msimamo wake wa awali, basi TUME, itafaanya maamuzi ya Mwisho katika kikao chake chenye akidi iliyokubalika kisheria. Maamuzi hayo yatasainiwa na Makamishina waliolisikiliza shauri husika na yatakuwa hitimisho la shauri husika kwa ngazi ya TUME.
- 14.9** Maamuzi ya Mwisho (Final Findings) ya TUME, yatawasilishwa kwa Wahusika na nakala moja itatolewa (baada ya kuzingatia masharti ya

usiri wa taarifa) na kuchapwa katika Gazeti la Serikali na katika Daftari la (rejista) umma la tovuti ya TUME.

14.10 Maamuzi ya Mwisho ya TUME (Final Findings) yataweka bayana adhabu au jinsi ambayo Kampuni husika itajirekebisha, sababu za uamuzi wa Tume na itaweka baya muda wa kisheria ambao Walalamikiwa wataweza kukata rufaa katika baraza la Ushindani (FCT) (yaani ndani ya siku 28). Ikiwa hakutokuwepo na rufani yoyote, basi, TUME itakuwa na sababu ya msingi ya kutekeleza uamuzi wake.

15.0 Mchakato wa Maridhiano

15.1 Mlalamikiwa (Mtuhumiwa) yeyote anaweza kuwasilisha maombi mbele ya TUME akiomba nafasi ya kulishughulikia shauri kwa njia ya majadiliano ya kutaka maridhiano.

15.2 Mchakato wa kuomba majadiliano ya maridhiano na TUME, utaanza tu mara baada ya TUME kufikia na kutoa '**Maamuzi ya Awali**' na si vinginevyo.

15.3 Kila taasisi ya biashara inayotafakari kuingia katika majadiliano na TUME ilikumaliza shauri la kiushindani linaloikabili itapatiwa rasimu ya adhabu/gharama za usuluhishi /maridhiano (settlement fees). Hata hivyo, hesabu ya gharama husika (settlement fees) yaweza kutofautiana katika kila shauri (kesi) kwa kuzingatia jambo linalohusika. Hili ni muhimu ili kuhakikisha kwamba rasimu husika inakidhi malengo ya adhabu ambayo TUME ingetoa kama shauri lingefikia mwisho.

15.4 TUME itatoa pia nafasi kwa Kampuni au mhusika ya kuwasilisha, ndani ya kipindi cha muda maalum, maoni yake kuhusiana na gharama husika ya maridhiano hayo (settlement fees) kama itakavyoonyeshwa katika rasimu ya maridhiano. Hata hivyo, yote haya yatafanyika ikiwa Mhusika anakubaliana kuwa kitendo kilichotendwa ni kinyume na sheria ya ushindani kama itakavyokuwa imebainishwa katika Maamuzi ya Awali ya TUME.

15.5 Ikiwa majadiliano ya maridhiano yatafanyika, majadiliano hayo yatafanyika ndani ya siku 45 tangu tangu tarehe ya kufunga uwakilishi wa utetezi wa mdomo. Kama majadiliano ya maridhiano yatashindwa kuendelea hadi mwisho, au kama Mtuhumiwa atajittoa katika

mchakato wa majadiliano, basi, mchakato wa utekelezaji wa sheria
utaendelea na kukamilishwa ndani ya siku 15.¹

TUME YA USHINDANI

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

© 2017.

¹ Taz. Kanuni za Tume, 2013, kif.cha 25(2) na (3).